# MUHTASARI WA RIPOTI YA ALMA - ROBO YA PILI, 2025

## UTANGULIZI:

Miaka 80 kamili iliyopita, mnamo mwezi Juni baada ya kumalizika kwa vita ya pili ya dunia; asilimia 80 ya idadi ya watu duniani takriban bilioni 2.3 walipitisha kwa kauli moja Mkataba wa Umoja wa Mataifa, ambao ulianza kutumika miezi michache baadae kuanzia mwezi Oktoba 1945. Kila nchi mwanachama ilitakiwa kukuza amani, maendeleo na haki za binadamu. Leo, karibia asilimia 100 ya idadi ya watu ulimwenguni wapatao bilioni 8 ni sehemu ya Umoja wa Mataifa. Ni matarajio ya kila raia kwamba mwaka huu, Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa - UNGA unapopitisha kaulimbiu ***"Bora Tukiwa Pamoja";*** serikali zote zitahakikisha kuwa haki za kila mwanamke, kila mwanaume, kila kijana, na kila mtoto zinalindwa, ili kuhakikisha uwepo wa amani na maendeleo endelevu.

## WANAWAKE NA WATOTO WA AFRIKA


Haki ya afya, ni moja ya hitaji muhimu na la msingi kwa binadamu. Afya na ustawi hutumika kama msingi imara wa maendeleo na kujenga amani. Malaria, ugonjwa ambao unazuilika na wenye tiba madhubuti, bado unasalia kuwa ni sababu kuu ya maradhi, vifo na maendeleo duni barani Afrika. Mwaka 2023, kulikuwa na wagonjwa milioni 246 wa malaria barani Afrika; milioni 12.4 kati yao wakiwa ni wajawazito. Mwaka huo huo, kulikuwa na vifo 569,000 vilivyotokana na malaria; kati ya hivyo, vifo 432,440 vilikuwa ni watoto umri chini ya miaka 5. Mmoja wa watoto hao alikuwa Mariama mwenye umri wa miaka 3 (zawadi ya mola) toka mji wa Kabala nchini Sierra Leone. Mama yake Mariama alikuwa ni mjamzito wakati huo; na kwa bahati nzuri alikuwa amepewa tiba-kinga toka kliniki, ili kuzuia athari za malaria kwa mama mjawazito (IPTp).

## BORA TUKIWA PAMOJA – UANZISHWAJI KWA KASI WA TEKNOLOJIA MPYA

Mama Mariama alikuwa na mtoto wa kiume anaitwa (Mohamed) aliyezaliwa baada ya kumpoteza Mariama. Analazimika kuhudumia bustani yake ya mboga-mboga huku akiwa amembeba Mohamed mgongoni, na anaenda nae sokoni ili kuuza mazao yake. Analala naye ndani ya chandarua kipya. Mariama alikuwa amelala ndani ya chandarua cha zamani chenye aina moja ya kiuatilifu pale alipopata malaria.

**WANACHAMA**
Algeria
Angola
Benin
Botswana
Burkina Faso
Burundi
Cameroon
Jamhuri ya Afrika ya Kati
Cabo Verde
Chad
Comoros
Jamhuri ya Congo
Ivory Coast
Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo
Djibouti
Egypt
Equatorial Guinea
Eritrea
Eswatini
Ethiopia
Gabon
Ghana
Guinea
Guinea Bissau
Kenya
Lesotho
Liberia
Libya
Madagascar
Malawi
Mali
Mauritania
Mauritius
Mozambique
Morocco
Namibia
Niger
Nigeria
Rwanda
Sahrawi Arab
Jamhuri ya Kidemokrasia ya São Tomé na Príncipe
Senegal
Seychelles
Sierra Leone
Somalia
Afrika Kusini
Sudan ya Kusini
Sudan
The Gambia
Togo
Tunisia
Uganda
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Zambia
Zimbabwe

**Aina ya viuatilifu vyenye usugu kwa mbu vilivyothibitishwa tangu mwaka 2010**





**Chanzo: Robo ya 2, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA**.
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*

Kwa bahati mbaya, chandarua hicho cha zamani kilimlinda kwa sehemu tu mtoto wake wa thamani kwa vile mbu mwerevu walishajenga usugu kwa viuatilifu.

Mnamo Aprili 2024 wakati serikali ilipoanzisha chanjo ya malaria, Kabala ilikuwa miongoni mwa wilaya 15 zilizolengwa kupata chanjo, kuanzia watoto wenye umri wa miezi 6. Mohamed alikuwa na umri sahihi. Hivyo alikuwa mmoja wa watoto wa mwanzo nchini Sierra Leone kupokea chandarua kipya chenye viuatilifu aina mbili venye ufanisi mkubwa.

Kufanya kazi wote kwa pamoja, kote ulimwenguni, vyandarua venye ufanisi mkubwa vimetengenezwa ili kukabiliana na usugu. Wadau waliungana pamoja ili kuharakisha kuanza matumizi ya vyandarua hivyo, kumeongeza kasi ya usambazaji kama ilivyoonekana mwaka 2025. Hata hivyo, sio nchi zote zimeweza kuanzisha kikamilifu matumizi ya vyandarua hivi vipya na vyenye ufanisi zaidi. Ingawa kupitishwa mapema kwa teknolojia mpya (k.m. chanjo ya malaria na chandarua kipya chenye aina mbili za viuatilifu) kulisaidia kumuokoa mtoto wake kutokana na malaria; kuchelewa kuanza kutumika kwa vyandarua hivi duniani kote kumechangia kumpoteza Mariama. Ni lazima tujifunze, na kuharakisha kuanza matumizi ya zana na teknolojia mpya kabla athari za viuatilifu, dawa na vipimo vya uchunguzi husababisha kuongezeka kwa ugonjwa wa malaria na vifo, ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa dawa mpya za kutibu malaria.


**Nchi zilizoanza kutumia Chanjo ya Malaria**



Matumizi ya chanjo ya malaria yameanza
Haihusiki
Hamna Takwimu

**Chanzo: Robo ya 2, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA**.
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*

**Asilimia ya Udhibiti wa vekta kwa mwaka jana nchi zilizokuwa na nyenzo mpya zenye ufanisi zaidi**



**Chanzo: Robo ya 2, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA**.
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*


## BORA TUKIWA PAMOJA – KUFANYA KAZI PAMOJA NA JAMII

Ubora wa kadi za alama kwa huduma za jamii ambazo huileta pamoja jamii ili kutambua na kujadili changamoto za upatikanaji wa huduma za afya; zinaonesha ufanisi kwa jamii inayofanya kazi pamoja na serikali, wawakilishi wao katika manispaa na mabunge. Kadi hizi za alama za jumuiya husaidia kufuatilia utendaji wa viashirio muhimu ikijumuisha:

- Huduma ya afya inayojali, yenye heshima na huruma
- Muda wa kusubiri huduma
- Upatikanaji wa dawa, vifaa na huduma
- Usimamizi wa gari la wagonjwa na rufaa
- Vituo vya afya vilivyo safi na salama
- Miundombinu ya kituo

Kama mfano, changamoto katika kushughulikia kuisha kwa bidhaa hutambuliwa mapema na kuchukua hatua za kurekebisha ikiwa ni pamoja na kuongeza mgao katika bajeti.

**Dawa-Mseto zilizopo (zinatosha kwa zaidi ya miezi 6)**





**Chanzo: Robo ya 2, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*

## BORA TUKIWA PAMOJA – MABARAZA NA FEDHA YA KUTOKOMEZA MALARIA NA MAGONJWA YA KITROPIKI YALIYOKUWA HAYAPEWI KIPAUMBELE


Wadau nchini, ikijumuisha sekta za serikali, viongozi wa sekta binafsi za viwanda, viongozi wa jumuiya, viongozi wa dini, washirika wa maendeleo, viongozi wa vijana na AZAKi wanafanya kazi kwa pamoja katika ngazi mbalimbali, ili kuharakisha ajenda ya kudhibiti na kutokomeza malaria na magonjwa ya kitropiki yaliyokuwa hayapewi kipaumbele - NTD. Zaidi ya dola za kimarekani milioni 166 zikiwa ni michango ya kifedha na isiyo ya kifedha imehamasishwa, kwa kutumia zana za kadi ya alama ili kusaidia kutambua vipaumbele katika uhamasishaji wa rasilimali.

**Mabaraza na Mifuko ya Kutokomeza malaria na Magonjwa ya Kitropiki yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele yaliyozinduliwa**




**Chanzo: Robo ya 2, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*


**Kufikia lengo la kupunguza visa vipya vya malaria kwa angalau asilimia 63 ifikapo mwaka 2023 (kulinganisha na 2015)**




**Chanzo: Robo ya 2, 2025 Kadi ya Alama ya Tathmini na Uwajibikaji ya ALMA.**
*Uteuzi na namna ya nyenzo zilivyowasilishwa katika ramani hizi, hauna uhusiano wowote na maoni ya uongozi wa ALMA kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au eneo la mamlaka yake au kuhusu uwekaji mipaka au mipaka yake.*

## BORA TUKIWA PAMOJA – MATUMIZI KAMILI YA USIMAMIZI WA KADI YA ALAMA

Utumiaji wa takwimu bora katika kufanya maamuzi umeonekana kuboresha usimamizi wa programu na utoaji wa huduma.




Kadi ya alama ya jamii, inasaidia katika kufanya maamuzi ya serikali na washirika; kusaidia kushawishi muundo wa programu na utoaji wa huduma. Inaathiri uwekezaji rasilimali na inaweza kuunganishwa moja kwa moja na kadi za alama za programu (malaria, lishe, kadi za alama za Afya ya Uzazi, Uzazi, Mama, Mtoto, Mtoto na Vijana) katika ngazi ya kituo cha huduma, wilaya/mikoa na ngazi ya taifa. Nchi zinahimizwa kufuata kwa kina mbinu hii ya kadi ya alama, ili kuongeza ubora wa takwimu za afya kwa ujumla, kuboresha matokeo ya afya, na kuleta usawa wa huduma za afya ikiwa ni haki ya binadamu na nguzo muhimu ya maendeleo.

## BORA TUKIWA PAMOJA - USHINDI KWA WOTE

Kuwekeza katika afya kupitia utekelezaji wa pamoja ambao unazingatia takwimu na uwajibikaji uliopangwa, hutoa matokeo na athari chanya kwa sekta zote na kwa wadau wote. Uwekezaji kwenye malaria unaonesha hili kwa uwazi kabisa. Mbinu ya kutumia kadi ya alama sio tu kuwa inaboresha utendaji, bali pia inaleta ufanisi na matumizi ya rasilimali yenye kuzingatia uchumi. Kuna uhaba wa rasilimali fedha duniani. Kila dola iliyowekezwa katika malaria kupitia mbinu hii ina uhakika wa kupata faida kubwa zaidi katika suala la udhibiti na kutokomeza magonjwa, kuongeza tija katika sekta zote, na kupunguza matumizi ya huduma za hospitali na rasilimali kwa maeneo mengine ya magonjwa. Uchambuzi wa Oxford umeonesha kuwa kufikia malengo ya kupunguza malaria ifikapo mwaka 2030 kunaweza kuongeza biashara ya kimataifa kwa dola za kimarekani bilioni 80.7. Tunasema hii itaokoa maisha ya akina Mariama wasiopungua 432,440 kila mwaka, na kuwapa maisha bora na yenye tija zaidi Waafrika milioni 246, wakiwemo wajawazito milioni 12.4 kila mwaka. Hiyo ni faida kubwa ya kupongezwa kwenye uwekezaji.